JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI**

**Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji S.L.P 218, Bariadi**
**Simu : +255(0)282700554, Tovuti : www.bariaditc.go.tz**
**Barua pepe : info@bariaditc.go.tz**
**Mawasiliano yote ya kiofisi yanayohusu HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI yatumwe kwa Mkurugenzi.**

---

# TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi anatangaza nafasi ya kazi moja **(1)** ya ajira ya mkataba wa mwaka mmoja. Maombi ya nafasi hiyo yanakaribishwa kutoka kwa Watanzania wenye sifa zilizotajwa katika tangazo hili.

Nafasi iliyotangazwa ni :-

1. **DEREVA WA MITAMBO: Nafasi 1**

***Majukumu:-***

(i) Kuendesha mitambo kikamilifu bila kusimamiwa

(ii) Kuweka vipimo mbalimbali vinavyotakiwa kufuatana na kazi anayofanya na jinsi anavyoelekezwa na kiongozi wake.

(iii) Kutoa huduma ya kwanza ya matengenezo ya mitambo na pia aweze kutoa maelezo sahihi ya ubovu wa mitambo anapotakiwa kufanya hivyo.

(iv) Kuandika vizuri 'log sheet' na kuweka kumbukumbu sahihi ya matumizi ya vifaa kwa mfano mafuta.

***Ngazi ya Mshahara: TGOS A***

***Mwombaji awe na sifa zifuatazo:-***

Kuajiriwa wenye cheti cha Kidato cha IV ambao wana leseni Daraja ' G' ya kuendesha mitambo na ujuzi wa kutunza vyombo mbalimbali vya mitambo hiyo, wenye uzoefu wa kuendesha mitambo kwa muda usiopungua masaa (300) mia tatu (3) bila kusababisha ajali.

***Sifa nyingine za Jumla:***

(i) Mwombaji awe raia wa Tanzania

(ii) Awe na umri wa kati ya miaka 18 na 40.

(iii) Maombi yake yaambatishwe picha (passport size) na vielelezo vya sifa zake

(iv) Mwombaji jinsia ya kike atapewa kipaumbele.

**Maombi yote yatumwe kwa:-**

Melkizedeck O.Humbe
Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji
S.L.P. 526
BARIADI

MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
BARIADI

Tangazo hili limetolewa leo tarehe **13.01.2021**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **27.01.2021 saa tisa na nusu (9 :30) Alasiri.**